
# Uhandisi



**“Galaxy Express”**

**Chuo cha Bibilia cha Likizo**






Kijitabu cha kituo cha ufundi

# Jopo la urambazaji

| | | |
|---|---|---|
| Itana kwake Mungu!<br>**Kuzaliwa kwa Musa**<br>Mungu ni Mkuu | Wakati wa somo hili, kila wakati wanafunzi wanaposikia "Mwite Mungu," ruhusu waitikie kwa kusema: "Bwana, Nisaidie!" Huku wakiruka na kuinua mikono yote miwili kuelekea kwa Mungu. | *“Kwa sauti yangu namwita BWANA Naye aniitikia toka mlima wake mtakatifu.” Zaburi 3:4* |
| Itikia kwake Mungu<br>**Musa na Kichaka kilicho kuwa kina chomeka**<br>Mungu ni Waajabu | Wakati wa somo hili kila mara wanafunzi wanapo sikia haya maneno “Itikia kwa Mungu ‘wafanye wajibu kwa kusema “Ndio Bwana” huku wakiweka mikono yao kwa sikio. Kisha wanagongesha miguu yao pamoja kama askari huku wakisema “hapa nipo!”. | *“Nimtume nani, naye ni nani atakaye kwenda kwa ajili yetu? Ndipo niliposema, Mimi hapa, nitume mimi” Isaya 6:8* |
| Tii Mungu<br>**Tauni zilizo kuwa misri**<br>Mungu ni Wakustaajabisha | Kila wakati wanafunzi wanaposikia "Mtii Mungu" wakati wa somo, ruhusu wanafunzi kujibu kwa kusema " Mimi lazima nisonge mbele " huku wakisimama na kubadilishana viti na wanafunzi wengine. | *“Naye azishikaye amri zake hukaa ndani yake yeye naye ndani yake. Na katika hili tunajua ya kuwa anakaa ndani yetu, kwa Huyo Roho aliyetupa.” Waraka wa kwanza wa Yohana 3:24* |
| Ngojea Mungu<br>**Wingu la kuwakinga na jua wakati wa mchana na nguzo la moto kuwapa joto wakati wa usiku**<br>Mungu ni Wakushangaza | Kila wakati wanafunzi wakisikia "Ngojea Mungu" wakati wa somo, wanafunzi wajibu kwa kusema "Niko tayari" huku wakiruka juu na kufanya ndondi, na kisha kusema "lakini mimi lazima nisubiri" wakiweka mikono yao pamoja na kukaa chini. | *“Kwa maana Bwana ni Mungu wa hukumu; heri wote wamngojao.” Isaya 30:18* |
| Abudu Mungu<br>**Kuvuka bahari ya Shamu**<br>Mungu ni Wakutisha | Kila wakati wanafunzi wakisikia "Mwabudu Mungu" wakati wa somo, wanafunzi wajibu kwa kusema "Ninakuabudu" huku waki inua mikono yao juu katika anga na kukitikisa mbele na nyuma. | *“Msifuni Mungu katika patakatifu pake; Msifuni katika anga la uweza wake.” Zaburi 150:1* |





www.ChildrenAreImportant.com - Rasilimali Za Huduma Ya Watoto, Shule Ya Jumapili na Chuo Cha Biblia Cha Likizo (VBS) Mtaala kwa Makanisa na Walimu. Swahili


| Chumba cha maamkuli | Darasa la Kadeti | Uhandisi | Michezo ya Anga |
| --- | --- | --- | --- |
| **Roboti**<br><br>Darubini |  | Musa katika kikapu<br> | Unda neno<br>Mtihani wa Ladha |
| **Kichaka cha musa kilicho kuwa kina chomeka**<br><br>Ukubwa wa kushangaza |  | Kile kichaka kilicho kuwa kina ungua<br> | Mbio ya Kunywa ya Relay<br>Mbio za kukula ndizi |
| **Mapigo**<br><br>Miondoko |  | Vua viatu vyako<br> | Mitindo za ajabu ya Sauti<br>Kichwa gamu |
| **Nguzo za Wingu**<br><br>Roketi za anga |  | Roketi ya Galaxy Express<br> | Kugusana juu ya mti<br>kutengeneza piramidi |
| **Kuvuka Bahari katika Ardhi Kavu**<br><br>Supernovas |  | Kuvuka Bahari ya Shamu<br> | Kuangusha Marshmallow<br>Relay ya Keki |

# Uhandisi

## Kituo cha ufundi



"Mimi hapa, nitume mimi!"
Isaya 6:8

## Siku ya 1

### Musa katika kikapu

Yanayo hitajika:
Picha ilio tayari (Chapa, kata, na toboa mashimo)
Krayoni (au penseli za rangi, kalamu zarangi , au rangi)
Maelezo:
1. Wanafunzi waandike majina yao nyuma na kupaka rangi mbele.
2. Wanafunzi wapitishe kamba ndani ya mashimo.




## Siku ya 2

### Kile kichaka kilicho kuwa kina uungua

Vifaa vya kutumia:
Nakala ya picha Kwa kila mwanafunzi
Vipande vidogo vilivyo raruka vya tishiu
Penseli za rangi
Maelekezo
1. Tengeneza nakala za kichaka ama uwaache watoto waji choree kichaka.
2. Paka matawi rangi ya hudhurungi (maji ya kunde).
3. Kusanya pamoja karatasi za tishiu, zungusha karatasi kwenye kijiti ama penseli ya rangi ama kwa kalamu,kisha finyilia kwenye tone la glue kwenye picha ili uunde matawi na miale.
4.Watoto pia wanaweza chora vitu vingine kwenye picha zao kama vile mawe, korongo, jangwa, milima,jua, mawingu, n.k  Kama unao muda wacha wanafunzi wako wawe wabunifu.



## Siku ya 3

### Vua viatu vyako


Vifaa:
Karatasi , Uzi au kamba, mbili kwa kila mwanafunzi , chombo cha kutoboa, Makasi, kalamu , kalamu ya alama.



Maelezo:
1. Chora mguu wa mtoto ( watoto wanaweza kutumia miguu ya kila mmoja kuchorea. ) Kwenye karatasi au povu .
2. Kata sura ya kiatu , toboa mashimo ya kuweka kamba .
3. Patia kila mtoto vipande viwili vya uzi ili kufungia viatu miguu zao.
Msiwe na wasiwasi ya kufanya kuwa kamilifu. Watoto wadogo hupenda kufunga kamba na inawafundisha misuli ndogo uratibu. Watoto wakubwa hufurahia kutumia kamba ndefu na kufunga viatu vyao vizuri.
4. Andika yafuatayo juu ya viatu : Nitamjibu Mungu, "Ndiyo Bwana, Mimi hapa. "

## Siku ya 4

### Roketi ya Galaxy Express



Vifaa:
* Nakala ya mfano wa roketi kwa kila mwanafunzi.
* Makasi (Kama wanafunzi watakata roketi zao wenyewe. Watoto wadogo wanahitaji mwalimu kuwakatia roketi zao hivyo wao ni kuunda tu.)
* Crayons au penseli za rangi
* Tape au gamu
Hiari: Tumia bomba tupu la karatasi ya choo.
Hiari: Shikisha nyota au vipande vidogo vya alumini kuongeza urembo.

Maelezo:
1. Kata vipande zote katika mistari yote imara.
2. Paka rangi kila sehemu.
3. Pindua "Galaxy express" iwe bomba kisha funga na mkanda au gamu ili ishikke.
4. Mabawa yakona vidude yakushika chini ya roketi. Elewa zinapitana ili iungane kabla ya kuingia ndani ya mwili wa roketi.
5. Kama unatumia bomba la karatasi ya choo, ingiza na upole kisha pindua na ukunje kwenye sehemu ya mabawa kabla kushikisha na koni huko juu.
6.Tengeneza koni, ukipishana hadi mstari ulio na alama. Funga na mkanda au gamu ishike juu ya roketi.

## Siku ya 5




### Kuvuka Bahari ya Shamu


Vifaa:
Karatasi nyeupe uliochapishwa aya au nakala ulio na bahari. Crayons za buluu, penseli za rangi, za alama, au rangi.


Maelezo:
1. Paka rangi sehemu ya maji na nchi kavu.
2. Kata au pasua kwenye mashimo ya mistari, simama kabla ya kufikia sehemu ya nchi kavu.
3. Zungusha vipande kwenye fimbo na ukase, penseli, au crayon. Ni hiari: paka Gundi mawe kidogo yenye ndani ya bahari.







Kwa sauti yangu
namwita BWANA
Zaburi 3:4



Kwa sauti yangu
namwita BWANA
Zaburi 3:4




"Mimi hapa, nitume mimi!"
Isaya 6:8



"Mimi hapa, nitume mimi!"
Isaya 6:8



Galaxy Express
Galaxy Express



“Msifuni Mungu

katika patakatifu

pake;

Msifuni

katika anga

la uweza

wake.”

Zaburi 150:1

Uhandisi

# Mawazo ya Ziada

## Ufundi wa ziada



Picha hii imeundwa na glue na kupakwa rangi ya unga au pambo. Inaweza kuwakilisha mlipuko wa furaha na sifa, kama ilivyo supanova! Ni furaha tunayo hisi wakati tunapo fikiri vile Mungu alivyo na yale ametenda kwa ajili yetu.
Maelezo yanaweza sema, "Nitamwabudu Mungu."

Shughuli Darasani

Kila mtoto atengeneze wingu lake mwenyewe, na darasa liunganishe nguzo binafsi la wingu la kila mmoja . Ili kuunda mawingu, waruhusu waichore, kisha wakate , na kuweka pambo kwa glue. (Unga nyeupe kutoka sokoni au pambo.) Rudia kwa safu ya miale ya moto.




Shughuli za ufundi: picha ya dunia kama inavyo onekana angani.
1. Chora duara kubwa katikati ya karatasi taulo kwa kutumia kalamu nyeusi au kalamu ya rangi isiyofutua na maji.
2. Wape wanafunzi kalamu zilizo na rangi za kijani ili wapake dunia rangi. Kisha wapake maji na kalamu ya rangi ya (samawati) bluu.
3. Sasa ruhusu wanafunzi wapake na maji. Wanahitaji kutia duara nzima maji na kutazama rangi ikichanganyika.
4. Mara inapo kauka, wanafunzi wakate kwenye mstari mweusi na kuweka glue ili washikanishe ubunifu wao kwa karatasi nyeusi.

## Class Activity





Hapa kuna ufundi wa ziada wa kufurahisha unaweza kutumia! Kupamba fimbo upande mmoja kama moto na upande wa pili kama nguzo la wingu!




Mavazi hayo yatakuwa ya ajabu kwa walimu wako kutumia ili kuongeza ladha ya VBS yako! Funika lita 2 ya chupa za soda kwa karatasi ya nailoni au cellotape ya rangi ya kijivu, shikisha na karatasi ya tishu iwe miale ya moto kisha ufunge kamba ili ifungiwe kwenye mgongo wako. Walimu wako watapendeza wakiwa wamevaa " mifuko ya jeti" !

Watoto wata PENDA kuwa na picha kutoka VBS yako!




## Shughuli: Bonde la mwezi


Ruhusu wanafunzi wako kujenga mchanganyiko wa unga, na kisha angusha mawe madogo ndani yake. Tazama bonde zikitokea, mbele ya macho yako!

Mchanganyiko wa Unga: vikombe 4 vya unga na 1/2 kikombe cha mafuta



Tafuta na utoe Raslimali zingine kwenye tovuti:

**www.ChildrenAreImportant.com/Galaxy**



Crafts Galaxy
Swahili
13656

www.ChildrenAreImportant.com
info@childrenareimportant.com
Tunapatikana Mexico.
DK Editorial Pro-Visión A.C.

Watoto ni wa muhimu